



Naibu Waziri wa Mambo ya ndani Mhe. Mhandisi Hamad Masauni ameipongeza hatua iliyofikiwa ya kusaini makubaliano kati ya RITA na Idara ya Uhamiaji katika utambuzi wa nyaraka kwa njia ya kidijitali ili kurahisisha utoaji wa huduma za vyeti vya kuzaliwa na pasi za kusafiria, ameyasema hayo hii leo Jijini Dar es salaam wakati wa Maadhimisho ya siku ya Kimataifa ya Wahamaji huku kukishuhudiwa utilianaji saini kwa Taasisi hizo mbili.

18 Desemba 2019 Toleo maalum

RITA NA IDARA YA UHAMIAJI KUFANYA KAZI PAMOJA YA UTAMBUZI WA NYARAKA ZA WANANCHI KIDIJITALI

Wakala wa Usajili Ufilisi na Udhamini (RITA) na Idara ya Uhamiaji zimesaini hati ya makubaliano ya kufanya kazi kwa pamoja ya utambuzi wa nyaraka kwa njia za kisasa za kidijitali ili kurahisisha utoaji huduma kwa wananchi wanaoomba vyeti vya kuzaliwa na pasi za kusafiria.

Akipongeza hatua hiyo hii leo Jijini Dar es salaam wakati wa maadhimisho ya siku ya kimataifa ya Wahamaji, Naibu Waziri wa Mambo ya ndani Mhe. Mhandisi. Hamad Masauni amesema kuwa hatua hiyo itarahisisha utoaji wa huduma kwa haraka kutokana na matumizi ya TEHAMA katika kuhakiki taarifa za wananchi wanaoomba pasi za kusafiria.

Mhandisi Masauni ameongeza kuwa makubaliano hayo ni jitihada za Serikali kuhakikisha Taasisi zote za umma zinafanya maboresho katika utoaji wa huduma zake kwa njia ya kidijitali na kumaliza malalamiko ya wananchi kucheleweshwa kupatiwa haki zao za huduma bora.

“Leo nimefurahi na nawapongeza RITA na Idara ya Uhamiaji kwa makubaliano haya na kuna kila sababu ya Taasisi nyingine za umma kujifunza kwa tukio hili ili kwa pamoja tuwaridhishe wananchi wetu kwa kuwapa huduma bora”. Alisema Mhandisi Masauni.

Kwa upande wake Kaimu Kabidhi Wasi Mkuu wa RITA Bi Emmy Hudson amesema ushirikiano uliopo kati ya Idara ya Uhamiaji na RITA ni wa muda mrefu hasa katika utambuzi wa nyaraka mbalimbali zinazohitajika

“Mara kwa mara huwa tunawasiliana na wenzetu wa Idara ya Uhamiaji kuthibitisha baadhi ya taarifa za wananchi wanaoomba huduma ya vyeti vya kuzaliwa hivyo leo kinachofanyika ni kuimarisha ushirikiano wetu kisheria ili tufanye kazi kisasa zaidi”. Alisema Bi Hudson.

Naye Kamishina wa Uhamiaji Dkt. Anna Makakala amesema ushirikiano uliokuwepo awali uliwezesha kubadilishana taarifa kwa njia ya makaratasi hivyo ilichangia kwa kiasi kikubwa kucheleweshwa utoaji wa huduma kutokana na nyaraka husika kufanyiwa utambuzi kwa njia ya kizamani.

“Kwa sasa Idara ya Uhamiaji tunatoa pasi za kusafiria kwa njia ya kielekroniki hivyo makubaliano haya ni muendelezo wa jitihada zetu za kutoa huduma kwa njia ya kidijitali”. Alisema Dkt Makakala.

Leo ni siku ya Kimataifa ya Wahamaji ambapo Mgeni Rasmi alikuwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani Mhe. Mhandisi Hamad Masauni huku mada mbalimbali zikiwasilishwa kuhusu umuhimu wa Wahamaji katika kukuza uchumi wa nchi na kupewa angalizo kwa baadhi yao wanaoingia kinyume cha sheria kuwa Idara ya Uhamiaji itaendelea kuwasaka na kuwachukulia hatua.

Picha za matukio ukurasa unaofuata

